

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA
SHINYANGA MHESHIMIWA ZAINAB R.
TELACK KWENYE KILELEL CHA
MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE
DUNIANI TAREHE 11/03/2017 KATIKA
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA
SHINYANGA**

*Kaimu Katibu Tawala Mkoa,
Meneja wa Benki ya CRDB,
Mganga Mkuu wa Mkoa Shinyanga,
Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa
Shinyanga,
Wafanyakazi wote wa Benki ya CRDB,
Wafanyakazi wa Hospitali ya Rufaa Shinyanga,
Wanawake wa Manispaa ya Shinyanga,
Wananchi wote,
Waandishi wa Habari,
Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana,*

Habari za Asubuhi:

Nianze kwa kuwashukuru sana akina mama kwa
kuitikia wito wa Benki ya CRDB Tawi la

Shinyanga kushiriki katika zoezi hili la kupima Afya zenu hususani Saratani ya Matiti na Shingo ya Kizazi.

Niishukuru Benki ya CRDB kwa kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuhakikisha inashughulikia suala la tiba na kinga kwa wananchi wake.

Nawashukuru pia Wafanyakazi wa Hospitali ya Rufaa ya Shinyanga kwa kutumia muda na taaluma yao kuokoa maisha ya akina mama hapa Shinyanga.

Ndugu Wananchi,

Wakati tunahitimisha maadhimisho ya siku ya wanawake duniani, ambayo kwa mwaka huu wa 2017 kaulimbiu yake inasema, “**Tanzania ya Viwanda, Wanawake ni msingi wa mabadiliko ya Kiuchumi**”, suala la Afya ya akina mama ni la kipaumbele cha juu sana. Ni vizuri wanawake kujua Afya zao mapema na kuwahi kupata tiba kwa wakati. Hii itawawezesha kushiriki vizuri katika shughuli za uzalishaji mali ambao utapelekea kuinua vipato vyao na familia zao.

Nashukuru leo hii Benki ya RCDB imeliona hili na kutumia nafasi hii kufadhili upimaji wa Saratani ya Matiti na shingo ya kizazi kama mchango wao kwa jamii hususani pale ambapo akina mama wanaposherehekea siku yao.

Ndugu Wananchi,

Jumla ya wanawake zaidi ya 400 wa Manispaa ya Shinyanga watashiriki zoezi hili litakalodumu kwa muda wa siku mbili. Ikumbukwe kuwa kujua Afya ni jambo moja na kuitunza na kupata tiba ni jambo jingine.

Ili utunze afya yako au upate tiba ya afya yako ni lazima ufanye maandalizi ya kujiwekea akiba ya fedha zako utakazotumia kwa ajili hiyo, hivyo shime kwa wanawake kutumia fursa nyingine ya Benki ya CRDB ya kufungua Akaunti ya Malkia ili kujiimarisha kiuchumi na hatimaye kukabiliana na changamoto za Afya zetu na familia kwa ujumla.

Mwisho, nawasihi wote kutumia fursa hii iliyotolewa na Benki ya CRDB kama mwanzo wa kuchunguza Afya zetu mara kwa mara na pia

kuwahamasisha wale ambao hawakubahatika kushiriki kwenye zoezi hili leo, kufanya hivyo pale inapowezekana. Pia nawaomba waandishi wa habari kutumia fursa hii kutoa elimu kwa wanawake juu ya umuhimu wa kupima afya zao hususani Saratani ya Matiti na Shingo ya Kizazi.

Baada ya kusema hayo naomba sasa niwakaribishe akina mama kwa ajili ya upimaji.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza